



Serikali imeamua kufanya miraa kuwa miongoni mwa madawa ya kulevya ya haramu ya daraja la C. Kupigwa marufuku kwa miraa kutaanza tarehe 24 Juni.

Kwa nini Miraa inapigwa marufuku?

Miraa ina viungo vya asili ambavyo vimo katika madawa yainayodhibitiwa kote Uingereza na kimataifa kwa sababu vina madhara. Kusaidia kulinda jamii kutokana na madhara ya kiafya na kijamii yanayotokana na miraa na kuhakikisha kuwa Uingereza haiwi kiini cha magendo ya miraa ya kimataifa. Itakuwa kinyume cha sheria kuzalisha, kumiliki, kusambaza na kuingiza ndani ya nchi au kutoa nje ya nchi bila ya leseni ya ofisi ya mambo ya ndani (Home Office).

Nini kitatokea kama utatumia miraa baada ya tarehe 24 Juni katika nchi za Uingereza na Wales?

Kuanzia tarehe 24 Juni 2014, polisi wataweza kutumia onyo la miraa na ilani ya adhabu ya kukiuka utaratibu (Penalty Notice for Disorder) ya £60 kwa mtu mzima. Hii ina maana kwamba, kama polisi watakupata na miraa ambayo ni ya matumizi yako binafsi, unaweza:

- Kupewa onyo kwa kosa la mara ya kwanza la kumiliki
- Kupewa ilani ya adhabu ya kukiuka utaratibu (faini ya £60) kwa kosa la mara ya pili la kumiliki
- Kukamatwa kwa kosa la mara ya tatu la kumiliki

Je, kupigwa marufuku kwa miraa kutahusisha sehemu za umma na binafsi?

Ndiyo. Miraa itakuwa ni dawa ya kulevya ya haramu ya daraja la C na hii itahusisha nchi nzima ya Uingereza.





Nini kitawatokea watakaokamatwa na miraa wenye umri wa chini ya miaka 17?

Vijana wenye umri wa miaka 17, au chini, hawawezi kupewa onyo la miraa au ilani ya adhabu ya kukiuka utaratibu (PND) kwa kumiliki miraa. Ibara ya 65 ya sheria ya uhalifu na ukiukaji utaratibu ya mwaka 1998 inahitaji kuwa vijana kama hao wapewe tahadhari ya vijana, tahadhari yenye masharti ya vijana au mashtaka.

Nini kitatokea kama utafanya biashara ya miraa baada ya kuwa madawa ya kulevya ya haramu ya daraja la C?

Kama utakamatwa, polisi watachukua hatua na kuna hatari ya kufunguliwa mashtaka. Kama dawa ya kulevya ya daraja la C itakuwa ni uvunjaji wa sheria kusambaza, kumiliki kwa azimio la kusambaza na kuingiza miraa nchini Vikwazo kwa makosa haya kwa madawa ya kulevya ya daraja la C ni pamoja na kufungwa kwa muda usiozidi miaka 14, faini isiyo na kipimo, au vyote viwili.

Kusambaza miraa kwa rafiki zako, hata kama unatoa bure, pia kunaeleweka kuwa ni 'kusambaza' katika sheria.

Ninaweza kuenda wapi kupata ushauri na msasada kuhusu kuacha kutumia miraa?

Kwa ushauri na maelezo kuhusu usaidizi na huduma za matibabu katika matumizi ya miraa, Daktari wako (GP) au ofisi ya wilaya (council) ni sehemu nzuri za kuanzia. Kwa ushauri wa siri na maelezo ya usaidizi na huduma za matibabu tafadhali tembelea

<http://www.talktofrank.com/need-support> au <http://www.nta.nhs.uk/who-service.aspx>